

SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE



OFFICE OF THE DEPUTY VICE CHANCELLOR
(ADMINISTRATION & FINANCE)

P.O. BOX 3000, CHUO KIKUU, MOROGORO, TANZANIA

TELEPHONE: +255 023 2603511-4, Direct +255 023 2604653

FAX: +255 0223 2604573. TELEGRAMS: UNIAGRIC - TELEX: 55308

E-mail: dvcadminfin@suanet.ac.tz

RECEIVED

DATE 24/07/2013

Kumb.Na. SUA/ADM/K.1/6 VOL.II

Tarehe: 16.07.2014

Wafanyakazi wote,
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,
MOROGORO

**Yah: UHAKIKI WA WANACHAMA NA UBORESHAJI WA VITAMBULISHO
VYA MFUKO WA AFYA YA JUMUIYA YA CHUO KIKUU CHA
SOKOINE CHA KILIMO (SCHF)**

Somo la hapo juu linahusika.

Katika mkutano wa 30 wa Kamati ya Kusimamia Mfuko wa Afya wa Jumuiya ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ulioketi tarehe 04 Juni, 2014 pamoja na mambo mengine kamati ilibaini kuwepo umuhimu mkubwa wa kubadilisha vitambulisho vya wanachama wa mfuko vinavyotumika kwa sasa ili kuviondoa kwenye matumizi "system" vitambulisho vyote ambavyo vimekuwa vinatumika isivyo halali.

Zoezi hili la kubadilisha vitambulisho linakwenda sambamba na uhakiki wa wanachama halali wa Mfuko kutokana na baadhi ya wanachama kujitoa na kujiunga na Mifuko mingine ya Afya. Aidha, zoezi hili pia ni utekelezaji wa Kanuni Na. 2.5 ya Mwongozo wa Mfuko wa Afya (SCHF), 2013 inayoelekeza kufanyika kwa uhakiki wa wanachama kila baada miaka mitatu.

Napenda kuwaarifu kuwa zoezi hili la kubadilisha vitambulisho litaanza rasmi tarehe 01 Agosti, 2014 kwa utaratibu ufuatao:-

1. Wanachama wote (Principal) watapaswa kujaza upya fomu za usajili ili kuhuisha taarifa zao. Fomu hizi zitapatikana kwenye Ofisi ya usajili wa wanachama na vitambulisho, Ofisi za wakuu wa Vitivo/wakurugenzi na Website ya SUA (sehemu ya Staff matters).
2. Fomu za usajili zitarejeshwa kwenye Ofisi ya Usajili wa wanachama na vitambulisho iliyoko jengo la Biashara la SUA zikiwa zimejazwa kikamilifu na kuambatishwa picha za wahusika kwa ajili ya hatua zaidi.
3. Kwa mujibu wa mwongozo wa mfuko wa Afya wa mwaka 2013, utaratibu wa usajili kwa wategemezi ni kama ifuatavyo:-

